

Kusaidia familia yako kukaa salama kwenye mtandao

Watoto wanaweza kujifunza, kuchunguza, kucheza na kupata marafiki kwenye mtandao. Lakini kunaweza kuwa na hatari.

Mtoto wako anaweza kuona maudhui yenye kukasirisha kimakosa, kuwasiliana na watu asiowajua au kudhulumiwa. Wanaweza pia kukosa mambo muhimu kama vile kutumia wakati nje.

Haya hapa ni baadhi ya mambo rahisi waweza kufanya ili kusaidia kuwaweka watoto salama kwenye mtandao.

Zungumza kuhusu usalama kwenye mtandao kama familia

Julisha mtoto wako kwamba anaweza kuja kwako kila wakati ikiwa kuna kitu kitatokea kwenye mitandao ambacho kitamfanya kuhisi hofu au kukasirika.

Wewe unaweza kumwomba mtoto wako kukuonyesha michezo na programu ambazo anatumia. Tumia mazungumzo ya eSafety [ya watu wanaoanza](#) ili kukusaidia wewe kuanza.

Weka sheria za familia pamoja

Kama familia, wewe unaweza kuchagua baadhi ya sheria rahisi ili kusaidia kuweka kila mtu salama kwenye mtandao. Unaweza kujumuisha vitu kama vile vifaa vinavyoweza kutumika, michezo na programu ambazo watoto wako wanaweza kutumia, na muda ambao unaweza kutumia kwenye mtandao. Vifaa na programu nyingi zina vipengele vya kuweka vikomo vya jinsi vinavyotumiwa. Tazama [video hii](#) ili kupata maelezo zaidi kuhusu uhibitaji na mipangilio ya wazazi.

Jua wapi unaweza kupata usaidizi

Ikiwa unahitaji usaidizi kuhusu suala la mtandao na huna uhakika wa kitu cha kufanya, zungumza na mtu ambaye unamwamini, kama vile rafiki au mwalimu katika shule ya mtoto wako. Unaweza pia kuzungumza na mtu kwa [Parentline](#) kwa msaada wa changamoto za malezi. Kamishna wa eSafety (eSafety) husaidia kuweka familia zote za Australia salama kwenye mtandao. Tovuti [ya eSafety](#) ina habari zaidi kuhusu [kuripoti unyanyasaji kwenye mtandao](#) na kuwa salama kwenye mtandao.



Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuweka familia yako salama kwenye mtandao, tafuta [eSafety kwa Wazazi](#) kwenye tovuti yetu. kwenye